**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA KILIMO**

# BODI YA KAHAWA TANZANIA

***(Imeanzishwa kwa Sheria ya Kahawa Namba 23 ya Mwaka 2001 na Marekebisho ya Sheria za Mazao Na. 20 ya mwaka 2009)***

# TAARIFA KWA UMMA

## MWONGOZO NA. 1 WA USIMAMIZI WA MASOKO NA MAUZO YA KAHAWA KWA MSIMU 2022/2023

### 1.0. UTANGULIZI

Bodi ya Kahawa Tanzania kwa kushirikiana na Tume ya Maendeleo ya Ushirika na Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala inatoa mwongozo wa mauzo ya kahawa kwa msimu wa 2022/2023 ambao utaanza mwezi Mei, 2022. Kwa mujibu wa kanuni ya 63 ya Kanuni za Tasnia ya Kahawa 2013. Bodi ya Kahawa Tanzania inatoa mwongozo huu ambao unatoa utaratibu wa masoko ya kahawa kwa msimu wa 2022/2023. Ifahamike kwamba, masuala yote ambayo hayakuelezwa katika mwongozo huu yataendelea kutekelezwa kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Tasnia ya Kahawa. Aidha, mwongozo huu unaweza kuboreshwa kwa kadri itakavyohitajika kwa mujibu wa Sheria na taratibu zilizopo (Sheria na miongozo husika inapatikana kwenye tofuti ya Bodi ya Kahawa Tanzania kupitia www.coffeeboard.or.tz)

### 1.1. Madhumuni ya mwongozo

Mwongozo unatoa maelekezo ya utaratibu wa usimamizi wa masoko na mauzo ya Kahawa kwa kuweka mazingira wezeshi kwa wakulima, wafanyabiashara na wadau wote kwa lengo la kuongeza ushindani, kuwezesha viwanda kupata malighafi, kupunguza malalamiko na ukiritimba usio wa lazima, kuimarisha bei ya mkulima na kuimarisha ushirika. Kwa kufanya hivyo kutaongeza ustawi na tija ya tasnia ya kahawa.

### 2.0. UTARATIBU WA MASOKO

Masoko ya kahawa yatafanyika kwa kupitia mifumo ya aina tatu ambayo ni soko la awali (*farmgate market/primary market*), soko la mnada na soko la moja kwa moja nje ya nchi (*direct export*).

## 2.1. Soko la awali

Kahawa itakayouzwa katika soko la awali ni kahawa iliyotayarishwa na mkulima na kuuzwa kama ghafi. Kwa robusta na arabika ngumu ni kahawa kavu ya maganda (dry cherry), kahawa safi ambayo haijapangwa kwenye madaraja (*Fair Average Quality-FAQ*) na kwa arabika ni kahawa kavu ya maganda (*parchment*).

### 2.1.1. Soko la awali kwa kahawa ya Robusta na Arabika ngumu

Kuanzia msimu 2022/2023 kahawa ya maganda ya Robusta na Arabika ngumu kwa Mkoa wa Kagera itakusanywa na kuuzwa kupitia Vyama vya Msingi vya Ushirika kwa uratibu wa Vyama Vikuu vya Ushirika na mauzo ya kahawa hizo utafanywa kwa kupitia njia zifuatazo;

#### 2.1.1.1. Mnada wa kahawa ya Robusta ya maganda (*dry cherry*) na Arabika ngumu (hard arabica)

Bodi ya Kahawa Tanzania kwa mujibu wa kanuni ya 42 ya Kanuni za Tasnia ya Kahawa 2013 itaendesha mnada wa kahawa ya maganda ambao utafanyika kila siku kuanzia saa tano asubuhi (Saa za Afrika Mashariki) mjini Bukoba mkoani Kagera. Aidha, Bodi ya Kahawa Tanzania kwa kushirikiana na Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala na Vyama Vikuu vya Ushirika kwa kushirikiana na Ofisi za Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya itabainisha maeneo ambayo yatakuwa yanaonesha mwenendo wa mnada kwa njia ya runinga (*screen*) kila wilaya ili kuwezesha wakulima kupata fursa ya kufuatilia mnada wa kahawa kila siku. Bodi ya Kahawa Tanzania baada ya mashauriano na Vyama Vikuu vya Ushirika itatengeneza kabrasha la mnada na kutuma kwa wanunuzi wa kahawa wenye leseni kwa njia ya barua pepe walizoziwasilisha na pia kwenye viwanda vya kukobolea kahawa.

#### 2.1.1.2. Mauzo ya kahawa ya Robusta ya maganda na Arabika ngumu moja kwa moja kwa wanunuzi wa kahawa

Wanunuzi binafsi wenye leseni wanaruhusiwa kununua kahawa ya robusta ya maganda moja kwa moja kutoka kwa vyama vya msingi kwa ushindani wa wazi kwa bei ambayo itakuwa si chini ya bei elekezi iliyotangazwa na Bodi ya Kahawa Tanzania kulingana na mwenendo wa soko. Bei hizo zitatangazwa kupitia tovuti ya Bodi ya Kahawa, radio, runinga, mbao za matangazo na simu za kiganjani au mitandao ya kijamii. Vyama vya Msingi vya Ushirika havina budi kutangaza kupitia Chama Kikuu cha Ushirika kiasi cha kahawa wanayotaka kuiuza kupitia mfumo huu na wanunuzi watashindana kupata kahawa hiyo. Katika utaratibu huu wanunuzi binafsi wanatakiwa kununua kiwango kilichopo kwenye ghala kwa ajili ya mauzo, kwa kuingia makubaliano ya ununuzi wa kahawa.

### 2.1.2. Ukusanyaji wa Kahawa ghafi kutoka kwa wakulima

Katika mfumo wa soko la awali, Chama cha Ushirika cha Msingi kitakuwa na wajibu wa kukusanya kahawa ghafi kutoka kwa wakulima kwa kuzingatia kanuni za kilimo bora cha kahawa kwa kufanya yafuatayo;

i. Kupima uzito wa kahawa ya maganda kwa kutumia mizani iliyohakikiwa na kuthibitishwa na Wakala wa Vipimo.
ii. Kutunza kumbukumbu na kumpatia mkulima stakabadhi inayoonyesha jina lake kamili, kiasi cha kahawa (kilo) zilizopokelewa, nambari za simu na akaunti ya benki pale mkulima anapokuwa nayo.
iii. Kufungasha kahawa kwenye magunia ya *vero* (gramu 250) na uzito wa kahawa ya maganda kwa kila gunia inapaswa kuwa kilo hamsini (50) na kuweka kwenye ghala lililothibitishwa kwa ushirikiano wa Chama Kikuu cha Ushirika na Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala kwa ajili ya mauzo. Katika kila gunia kutakuwa na nembo inayoonyesha sifa za kahawa na jina la mkulima na kama zitachanganywa majina ya wakulima wote yataorodheshwa.
iv. Kuhakikisha kuwa ghala la kuhifadhia kahawa kabla ya kuuzwa linakuwa katika hali ya usafi na kulindwa wakati wote ili kuhakikisha kahawa ya mkulima inakuwa salama na ubora wake hauathiriki kwa namna yeyote.
v. Kuandaa na kutoa taarifa sahihi ya kahawa iliyokusanywa na kuhifadhiwa kwenye ghala tayari kwa mauzo kila siku kabla ya saa kumi na moja jioni.
vi. Kuomba kibali cha kuuza kahawa kwa kujaza fomu ambazo zitapatikana kwenye Vyama Vikuu vya Ushirika, Ofisi za Bodi ya Kahawa za Kanda na kwenye tovuti ya Bodi ya Kahawa (www.coffeeboard.or.tz).

#### 2.1.2.1. Vigezo vya udhibiti ubora wa kahawa ya maganda

Vyama vyote vya msingi na watunza ghala wanatakiwa kuzingatia vigezo vifuatavyo vya kahawa ya maganda wakati wa ukusanyaji na upokeaji wa kahawa;

i. Kahawa ya maganda inayokusanywa inatakiwa kuwa na unyevu usiozidi asilimia 12.5 (12.5%MC)
ii. Kahawa za wakulima zinazopokelewa zinatakiwa kuwa hazijachanganywa na vitu visivyo kahawa (mawe, mchanga, maharage n.k).
iii. Kahawa zipimwe uzito na kuwekwa katika gunia la vero kwa kilo 50 lenye alama za utambulisho kwa kila Chama cha Msingi cha Ushirika.

#### 2.1.2.2. Upokeaji na Utunzaji wa Kahawa katika Ghala la Mnada

i. Mtunza ghala atatakiwa kupokea kahawa ghafi ya maganda zilizo katika ubora na unyevu wa asilimia 12.5 na kuzipanga katika loti tofauti za gunia 100.
ii. Mtunza ghala anatakiwa kuzingatia viwango vya udhibiti ubora kama ilivyoainishwa katika mwongozo huu.
iii. Mtunza ghala anatakiwa kuhifadhi na kuzitoa kahawa kwa mnunuzi husika zikiwa katika ubora na kiasi kama ilivyoainishwa katika mchanganuo wa mauzo.

iv. Mtunza ghala anatakiwa kuingiza taarifa za kahawa ya maganda zilizoingia ghalani kila siku kwenye mfumo wa kieletroniki wa Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala zinazohusiana na kiasi cha uzito, idadi ya gunia, kiwango cha ubora na mmiliki.
v. Mtunza ghala la chama cha msingi endapo atatoa taarifa ya kuandaa mchanganuo wa mauzo ambayo haiendani na ubora na kiasi cha kahawa kilichopo ghalani atahusika kulipia hasara itakayojitokeza kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za usimamizi wa Stakabadhi za Ghala.

### 2.1.3. Uendeshaji wa minada ya kahawa ya maganda ya robusta na arabika ngumu

Kwa mujibu wa taratibu za uendeshaji wa minada ya kahawa, minada ya kahawa kavu ya maganda itaendeshwa kwa utaratibu ufuatao;

i. Chama cha ushirika cha msingi kitaandaa taarifa ya kahawa inayotakiwa kuuzwa kwenye mnada ikionyesha kiwango cha unyevu (MC 12.5%), kiasi cha kahawa na ubora unaostahili.
ii. Chama kikuu kitathibitisha taarifa zilizotolewa na chama cha msingi kila siku kuanzia saa 11:00 jioni na kuandaa kabrasha la mauzo (*Sales catalogue*) na kisha kulituma Bodi ya Kahawa kwa ajili ya maandalizi ya mnada.
iii. Bodi ya Kahawa Tanzania kwa kushirikiana na Chama Kikuu cha Ushirika pamoja na Mwendesha ghala wataratibu uchotaji wa sampuli za kahawa kwenye maghala kwa ajili ya kudhibitisha ubora na kuoneshwa kwa wanunuzi siku ya mnada.
iv. Kahawa itauzwa kama vile ambavyo sampuli itakavyoonyeshwa siku ya mnada (*Sale as per sample*).
v. Wanunuzi wenye leseni watakaojitokeza siku ya mnada watasajiliwa na kupewa namba maalum na nywila (password) itakayowawezesha kushiriki kwenye mnada utakaoendeshwa kwa uwazi.
vi. Mnada utaendeshwa Bukoba mjini mkoani Kagera kwa muda wa masaa mawili kuanzia saa tano kamili asubuhi kulingana na upatikanaji wa kahawa.
vii. Vyama Vikuu vya Ushirika kwa kushirikiana na Bodi ya Kahawa Tanzania vitahakikisha kunakuwa na runinga (*Price tickers*) katika maeneo ya Wilaya/Vyama Vikuu zitakazoenesha mwenendo wa mnada ili wakulima waweze kufuatilia mauzo ya kahawa zao.
viii. Kiasi cha kahawa ambacho kitatangazwa na kuuzwa kupitia mnada wa wazi kitakuwa kuanzia tani 100 (sawa na gunia 200) na kuendelea.
ix. *Lot* moja ya kahawa ya maganda itakuwa ni jumla ya kahawa itakayokuwa kwenye AMCOS moja.
x. Baada ya mnada kukamilika wanunuzi ambao watakuwa wameshinda kununua kahawa watapewa hati ya madai (*invoices*) ya kahawa walizonunua ndani ya saa moja na watatakiwa kulipa ndani ya masaa 24.

Katika taratibu zote hizi za mauzo ya kahawa kwenye soko la awali, wanunuzi watatakiwa kuweka fedha za manunuzi ya kahawa kwenye akaunti ya Bodi ya Kahawa Tanzania ndani ya saa ishirini na nne baada ya

mnada. Aidha, Bodi ya Kahawa Tanzania baada ya kuondoa makato yote yaliyoainishwa itahamisha fedha zilizobaki kwenda kwenye Chama cha Msingi ndani ya masaa ishirini na nne (24) baada ya kupokea malipo.

xi. Wanunuzi wa kahawa katika Mkoa wa Kagera watatakiwa kuweka amana ya kiasi cha Shilingi Milioni 10 kwenye Akaunti ya Bodi ya Kahawa Tanzania mwanzoni mwa msimu. Mnunuzi atakayenunua kahawa na kushindwa kulipa ndani ya muda uliopangwa fedha ya amana itatumika kulipia kahawa aliyoinunua na atachukuliwa hatua ikiwa ni pamoja na leseni yake kusimamishwa. Fedha hizi zitarejeshwa kwa wanunuzi mara baada ya msimu wa kahawa kuisha.

xii. Mara baada ya malipo, mnunuzi atapata cheti cha kuondoa kahawa kwenye ghala (*Release order*) ambapo atatakiwa kuondoa ndani ya masaa 48 na kupeleka kwenye kiwanda alichokiainisha kwenye maombi ya Leseni ya ununuzi wa kahawa na kuiuza katika soko la mnada wa kahawa safi, viwanda vya kukaanga au kwa utaratibu wa soko la moja kwa moja kwa mujibu wa kanuni zinazosimamia Tasnia ya Kahawa.

xiii. Chama cha Msingi cha Ushirika kitaendelea kuhakikisha kahawa inabaki katika hali ya usalama kwa kuzingatia ubora na ulinzi ndani ya muda wa masaa 48 baada ya mauzo, na mnunuzi akishindwa kuondoa kahawa aliyonunua ndani ya muda huo atalazimika kuingia gharama za uhifadhi wa kahawa hiyo.

#### 2.1.4. Malipo kwa wakulima

Mara baada ya wanunuzi kulipa fedha za mauzo Bodi italipa Chama husika ambacho kinatakiwa kuwalipa wakulima kulingana na orodha ya wakulima iliyotumika kupokelea kahawa kwenye ghala. Malipo kwa wakulima yatakuwa kwa utaratibu wa mkulima aliyewasilisha awali ndio analipwa kwanza [First in First Out (FIFO)]. Malipo ya kahawa yatalipwa kupitia akaunti za wakulima waliouza kahawa hizo au moja kwa moja kwa wakulima kulingana na matakwa ya mkulima husika na malipo kwa wakulima yatazingatia bei iliyokubaliwa katika makubaliano ya mauzo ya kahawa kwa wanunuzi binafsi au bei iliyopatikana mnadani kuondoa makato yaliyokubaliwa na ya kisheria.

#### 2.1.5. Makato na tozo katika soko la awali (*Farmgate Market*) kwa Mkoa wa Kagera

Kuanzia msimu huu wakulima wa kahawa Mkoani Kagera watakuwa na tozo/makato ya aina tano na yatalipwa na mnunuzi wa kahawa. Tozo hizo ni kama ifuatavyo:

| Aina ya Tozo | Kiasi | Matumizi |
|---|---|---|
| Ushuru wa Chama cha Ushirika cha Msingi | Shilingi 70 kwa kilo | Kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za chama cha msingi. |
| Ushuru wa chama cha kikuu | Shilingi 30 kwa kilo | Kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Chama Kikuu cha Ushirika na utalipwa na chama cha msingi. |

| | | |
|---|---|---|
| Gharama za Magunia (Vero) | Shilingi 6 kwa kilo | Kwa ajili ya ununuzi wa magunia ya kuhifadhia kahawa katika vyama vya msingi. |
| Ushuru wa Halmashauri | Asilimia 3 ya Bei ya kahawa kwa kilo | Inalipwa na wanunuzi wa kahawa kwa Halmashauri za wilaya kwa mujibu wa sheria. |
| Mchango wa maendeleo ya zao | Shilingi 100 kwa kilo | Inakusanywa na Bodi ya Kahawa kwa ajili ya ya kugharamia shughuli mbalimbali za maendeleo ya zao la kahawa. |

### 2.2. Soko la awali kwa kahawa za arabika laini ya maganda (parchment)

Mauzo ya kahawa ya arabika laini ya maganda (*parchment*) katika soko la awali itakuwa kama ilivyokuwa katika msimu wa 2021/2022 ambapo wakulima kupitia vyama vyao vya msingi watauza kahawa ya maganda kwa wanunuzi binafsi baada ya kuingia nao makubaliano yanayoonesha bei iliyokubaliwa na kiasi cha kahawa kilichonunuliwa, au kukusanya kahawa mbivu (*ripe cherry*) na kuichakata kwenye mitambo midogo ya kuchakata kahawa (*Central Processing Units -CPUs*) kwa ushirikiano na sekta binafsi.

Wakulima wa kahawa ya arabika laini ya maganda watalipa kiasi cha Shilingi 200 kwa kilo ya kahawa kwa ajili ya kugharamia shughuli mbalimbali za maendeleo ya zao la kahawa ambayo itakusanywa na Bodi ya Kahawa Tanzania wakati wa mauzo.

### 2.3. Soko la minada ya kahawa safi

Kama ilivyokuwa katika msimu uliyopita Bodi ya Kahawa Tanzania itaendesha minada ya kahawa safi katika Kanda za uzalishaji kama ifuatavyo:

i. Kanda za Mbeya/Songwe – Minada ya kahawa itafanyika Wilaya ya Mbozi katika ukumbi wa kiwanda cha kukobolea kahawa Mbozi (MCCCo).
ii. Kanda ya Ruvuma - Minada ya kahawa itafanyika katika Wilaya ya Mbinga katika ukumbi wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mbinga.
iii. Kanda ya Kaskazini itaendelea kwa kuuza kahawa ya mikoa ya kanda ya Kaskazini na kahawa kutoka kwa wauzaji wengine watakaopenda kuendelea kutumia mnada huu.

Katika kipindi chote cha msimu minada itafanyika kila wiki siku ya Alhamisi na wauzaji katika Kanda zote wataruhusiwa kuuza kahawa yao kwenye mnada wowote watakaopenda ili kuwahi mzunguko wa mnada. Viwanda vya kukoboa kahawa vitatakiwa kuwasilisha kwenye Ofisi za Kanda za Bodi ya Kahawa Tanzania sampuli za kahawa pamoja na *warrant* angalau siku kumi kabla ya siku ya mnada ili kuiwezesha Bodi ya Kahawa Tanzania kufanya maandalizi ya minada. Aidha, viwanda vya kukoboa kahawa havitatakiwa kuchanganya kahawa za wanunuzi walionunua sehemu tofauti ili kulinda ubora wa kahawa wa sehemu husika.

## 2.4. **Soko la moja kwa moja (direct export)**

Kwa mujibu wa Jedwali la Tano la Kanuni za Tasnia ya Kahawa za mwaka 2013, wauzaji wa kahawa wenye nia ya kuuza kahawa kupitia soko la moja kwa moja watalazimika kufanya tathmini ya bei, kati ya bei ya kahawa ya daraja hilo kwenye minada na soko la dunia ikilinganishwa na bei iliyoahidiwa na mnunuzi (*Offered price*) kabla ya kuingia makubaliano ya ununuzi wa kahawa. Makubaliano ya kuuza kahawa kwenye soko la moja kwa moja yakishafikiwa na kusajiliwa na Bodi ya Kahawa Tanzania yanatakiwa kuheshimiwa kwa mujibu wa Sheria ya Mikataba ili kulinda taswira ya tasnia ya Kahawa nchini.

Aidha, wanunuzi wa kahawa kwenye soko la moja kwa moja watalazimika kuwa wamewasilisha makubaliano ya ununuzi wa kahawa Bodi ya Kahawa Tanzania kwa ajili ya usajili ndani ya siku 3 tangu kuingiwa kwa makubaliano hayo pamoja na sampuli ya kahawa kwa ajili ya tathmini ya ubora. Aidha, wanunuzi hao watalazimika kulipa malipo ya mauzo ya kahawa ndani ya muda uliokubaliwa kwenye mikataba yao. Muuzaji anatakiwa kulipa ankara yake ya kibali cha kuuza kahawa nje ya nchi ndani ya siku saba.

# 3.0. SOKO LA KAHAWA ENDELEVU (SUSTAINABLE AND CERTIFIED COFFEES)

Wazalishaji wa kahawa endelevu (*sustainable and certified coffees*) ambao tayari wamepata vyeti kupitia uratibu wa Vyama Vikuu vya Ushirika na kampuni zilizowekeza kwenye uzalishaji wa kahawa endelevu wataendelea na uratibu wa mauzo ya kahawa ya aina hii baada ya kuingia katika makubaliano ya kilimo cha mkataba (*contract farming*) kama ilivyoelekezwa kwenye Kanuni za Kahawa, 2013. Bodi ya Kahawa Tanzania inatoa maelezo haya ili kuendelea kulinda uwekezaji uliyofanyika na kuwezesha uwekezaji mpya endelevu kwenye mnyonyoro wa thamani na kutovunja utaratibu wa mauzo ya kahawa endelevu katika masoko maalum. Wauzaji wa kahawa endelevu wanashauriwa kuuza kahawa yao kupitia maghala ya Bodi ya Kahawa Tanzania yaliyosajiliwa katika kilimo endelevu.

# 4.0. UPATIKANAJI WA MAGUNIA NA VIFUNGASHIO

Wauzaji wa kahawa safi nje ya nchi watatakiwa kuhifadhi kahawa kwenye magunia safi (katani na Jute). Magunia yanayoagizwa nje ya nchi, ni lazima yawe na nembo inayoonesha kuwa yanafaa kutumika kwa kuhifadhia chakula (*food grade*). Aidha, viwanda vinatakiwa kuzingatia viwango vya magunia vilivyowekwa na Shirika la Viwango la Taifa (*Tanzania Bureau of Standards - TBS*).

Kila kiwanda kitakachoagiza magunia kitatoa taarifa na nakala ya ubora uliopitishwa na TBS kwa Bodi ya Kahawa Tanzania. Ikitokea kiwanda cha kukoboa kahawa kitatumia magunia yasiyokidhi vigezo na kuharibu ubora wa kahawa, kitalazimika kulipa fidia ya uharibifu utakaotokea.

## 5.0. UPATIKANAJI WA MALIGHAFI KWA WASINDIKAJI WA KAHAWA (WAKAANGAJI) WA NDANI

Ili kuongeza kiwango cha kahawa kinachoongezwa thamani kwa ajili ya soko la ndani na kuuzwa kwenye soko la nje, wasindikaji wa kahawa watapata malighafi kwa ajili ya usindikaji kwa kupitia njia zifuatazo;

i. Kununua kahawa kwenye minada (ya maganda na kahawa safi).
ii. Kununua kahawa ya maganda kutoka kwa vyama vya msingi kwa mujibu wa kipengele 2.1.1.2 cha mwongozo huu.
iii. Wazalishaji kahawa wenye mashamba makubwa yaliyosajiliwa wanaruhusiwa kusindika kahawa yao waliyoizalisha mara baada ya kuipeleka kwenye kiwanda cha kukoboa chenye leseni. Mzalishaji wa kahawa atatoa kwa Bodi ya Kahawa Tanzania taarifa ya kiasi cha kahawa kinachotengwa kwa ajili ya kuongezwa thamani na kinachoachwa kwa ajili ya kuuzwa.

## 6.0. WAJIBU WA WADAU KATIKA UTEKELEZAJI WA MWONGOZO

Ili kutekeleza mwongozo huu, wadau wa kahawa watakuwa na wajibu ufuatao;

### 6.1. Mkulima

i. Kutayarisha kahawa kwa ajili ya mauzo kwa mujibu wa kanuni za kilimo bora cha kahawa ikiwa ni pamoja na kuvuna kahawa iliyoiva, kuitayarisha katika ngazi ya awali (primary processing) kutokana na aina ya kahawa na kuihifadhi katika magunia safi.
ii. Kukusanya kahawa katika chama cha msingi kilichopo katika eneo lake.
iii. Kupokea hati ya kupokelewa kahawa kutoka chama cha msingi ikionyesha uzito wa kahawa na taarifa nyingine muhimu.
iv. Kufuatilia taarifa za mauzo ya kahawa kwenye chama cha msingi.
v. Kupokea malipo ya mauzo ya kahawa.

### 6.2. Chama cha Ushirika cha Msingi

i. Kuhakikisha kuwa mizani inayotumika kupimia kahawa imekaguliwa na Wakala wa Vipimo.
ii. Kukusanya kahawa kutoka kwa wakulima zenye kiwango cha unyevu usiozidi asilimia12.5 (MC 12.5%)
iii. Kuhakikisha upatikanaji wa magunia ya kuhifadhia kahawa inayokusanywa na wakulima.
iv. Kuhakikisha kila gunia linakuwa na nembo inayoonesha ubora wa kahawa na mmiliki au wamiliki wa kahawa hiyo.
v. Kuhifadhi kahawa ya wakulima kwenye magunia kwa uzito wa kilo hamsini.
vi. Kutoa hati ya kupokelea kahawa inayoonyesha kiasi cha kahawa kilichopokelewa.

vii. Kutunza kahawa na ubora wake kabla ya kuuzwa au kupelekwa kwenye kiwanda cha kukoboa kahawa.
viii. Kuweka kumbukumbu sahihi kwenye rejesta itakayosainiwa na mkulima au mwakilishi wake.
ix. Kuandaa kahawa inayotakiwa kupelekwa kwenye mauzo kwa njia ya mnada na kuwasilisha taarifa Chama Kikuu cha Ushirika kwa ajili ya maandalizi ya mauzo kila siku ifikapo saa kumi na moja jioni
x. Kuhakikisha malipo ya mkulima yanafanyika kwa wakati.
xi. Kuwa na vitabu vya kutolea stakabadhi pamoja na nyaraka za kusafirisha kahawa (PDN)

### 6.3. Chama Kikuu cha Ushirika

i. Kuratibu ukusanyaji wa kahawa unaofanywa na vyama vya msingi na kusaidia pindi changamoto za upokeaji wa kahawa zinapojitokeza.
ii. Kushirikiana na vyama vya msingi kuandaa kabrasha la mauzo kwa ajili kuendesha minada ya kahawa ya maganda ambayo itaonyesha taarifa muhimu za kahawa inayouzwa.
iii. Kutambua ghala zote zitakazotumika kwa ajili ya minada ya kahawa.
iv. Kuratibu usafirishaji wa kahawa.
v. Kuratibu na kusambaza vifungashio vyote.
vi. Kuhakikisha kuwa vifungashio vinavyotumika kuhifadhia kahawa vinakuwa na nembo maalum inayoonesha ubora wa kahawa na umiliki wake.
vii. Kwa kushirikiana na Bodi ya Kahawa Tanzania kuandaa ratiba ya minada na kuratibu uendeshaji wake.
viii. Kuratibu uzalishaji na mauzo ya kahawa endelevu (*Certified coffee*).
ix. Kuwa na vitabu vya kutolea nyaraka muhimu katika usafirishaji wa kahawa.
x. Kutoa taarifa za minada kwenye kila chama cha ushirika cha msingi.
xi. Kufanya shughuli nyingine kwa lengo la kurahisisha mauzo ya kahawa.

### 6.4. Wanunuzi wa kahawa katika soko la awali

i. Kununua kahawa katika masoko ya kahawa kama ilivyoainishwa katika mwongozo huu.
ii. Kufanya malipo ya ununuzi wa kahawa katika muda uliopangwa zikiwemo tozo mbalimbali kwa mamlaka husika
iii. Kulinda na kuhakikisha ubora unatunzwa wakati wote.
iv. Kuuza kahawa safi kwenye masoko yaliyoainishwa katika mwongozo huu.
v. Kuhakikisha kuwa wanazingatia masharti ya leseni zao.
vi. Kuweka fedha ya amana ya shilingi milioni 10 kwenye akaunti maalum ya Bodi ya Kahawa Tanzania
vii. Hairuhusiwi mnunuzi wa soko la awali kumuuzia kahawa mnunuzi mwingine wa soko la awali.

### 6.5. Msimamizi wa Ghala

i. Kutoa taarifa za uzito na ubora wa kahawa zilizopokelewa na kuhifadhiwa kwenye ghala husika zitakazosaidia kuandaa kabrasha la mauzo
ii. Kuhakikisha kuwa kahawa inayopokelewa katika ghala inakidhi viwango vya ubora.
iii. Kuhakikisha gunia zote zilizohifadhiwa kuwa na nembo inayoonesha ubora na umiliki wa kahawa husika.
iv. Kuhakikisha kuwa wanunuzi wanatoa mzigo kulingana na ubora, uzito na kwa mpangilio kwa mujibu wa taratibu
v. Kutoa taarifa ya mapokezi na uondoshaji wa kahawa kwa Chama Kikuu cha Ushirika, Bodi ya Kahawa Tanzania, Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania na Halmashauri za Wilaya.

### 6.6. Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala

i. Kusajili na kutoa leseni ya ghala za kuhifadhia kahawa za wakulima;
ii. Kuhakikisha ghala zote zinakidhi viwango vya kuhifadhi kahawa;
iii. Kupokea taarifa za kiwango na ubora wa kahawa zilizoingia ghalani kila siku; na
iv. Kufuata taratibu nyingine kama zilivyoainishwa kwenye mwongozo huu.

### 6.7. Bodi ya Kahawa Tanzania

i. Kusajili na kutoa leseni za ununuzi wa kahawa kwa wanunuzi wa kahawa
ii. Kuandaa na kutoa taarifa ya mwenendo wa soko la kahawa.
iii. Kwa kushirikiana na Vyama Vikuu vya Ushirika kuratibu uendeshaji wa minada ya kahawa ya maganda ya Robusta.
iv. Kupokea malipo ya mauzo ya kahawa na kuchakata malipo na kutuma katika akaunti za benki kwa mchanganuo uliokubaliwa.
v. Kuendesha minada ya kahawa ya maganda na kahawa safi katika kanda za uzalishaji.
vi. Kutoa hati ya kuondoa mzigo kwa wanunuzi (*Release Order*)

### 6.8. Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania

i. Kuhakikisha kuwa vyama vya ushirika vya msingi vina uwezo wa kufanya biashara ya kahawa ikiwa ni pamoja na uwezo wa kutunza kumbukumbu na vitabu vya mahesabu.
ii. Kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa vyama vya ushirika vya msingi ili kubaini mapema changamoto za kiutendaji za viongozi wa vyama na kuimarisha utendaji wa vyama vya ushirika.
iii. Kuhakikisha kuwa wakulima wanalipwa bei ya kahawa wanayostahili kulingana na mauzo ya kahawa yao.
iv. Kutoa mafunzo kwa makatibu wa vyama ili kujua wajibu wao na uelewa wa biashara ya kahawa.

### 6.9. Halmashauri za Wilaya

i. Kuelimisha, kusimamia na kuhamasisha wakulima kuuza kahawa kwa kufuata mfumo huu;
ii. Kudhibiti ununuzi wa kahawa holela usiofuata taratibu ikiwemo magendo ya kahawa;
iii. Kutoa vibali kwa wanunuzi wa kahawa ikiwa ni moja ya masharti ya kupata leseni;
iv. Kuhakikisha kuwa wakulima wanazingatia kanuni bora za kilimo katika uzalishaji na utayarishaji wa kahawa kwa ajili ya mauzo; na
v. Kuweka mazingira wezeshi wakati wa kusafirisha wa kahawa ambayo imeuzwa kutoka katika Halmashauri zao.

### 6.10. Sekretarieti za Mkoa

i. Kusimamia na kuhakikisha mfumo unafanya kazi vizuri kwa kuhakikisha kila mdau anatekeleza wajibu wake kwa mujibu wa mwongozo huu.
ii. Kushirikiana na Bodi ya Kahawa Tanzania na Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania katika kutoa elimu ya utekelezaji wa mfumo huu kwa wadau wote kwenye mnyororo wa thamani wa kahawa.
iii. Kufanya ufuatiliaji wa zoezi nzima la ukusanyaji, mauzo na malipo kwa wakulima na wadau wengine pamoja na usafirishaji wa Kahawa.

Imetolewa na:

…………………………
Mkurugenzi Mkuu,
Bodi ya Kahawa Tanzania,
S. L. P 732,
**MOSHI**.

…………………………………..
Mrajisi wa Vyama vya Ushirika,
Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania,
S. L. P. 201,
**DODOMA**

……………………………….
Mkurugenzi Mtendaji,
Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala,
S. L. P. 38093,
**DAR ES SALAAM**